# Ufutuhi katika Jamii za Watanzania: Mjadala kuhusu Sura za Utokeaji na Dhima zake

A.S. Ponera


## Ikisiri

Makala haya yanafafanua jinsi ufutuhi unavyojitokeza kwa jamii ya Watanzania pamoja na dhima zake. Ufutuhi unajadiliwa humu kama hali za uchangamfu, furaha, na kicheko inayojengwa na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto. Sura za utokeaji wa ufutuhi zinaoneshwa kupitia data 23 za ujumbe za kifutuhi zilizokusanywa kutoka katika vyanzo anuwai vya mifumo ya kimawasiliano itokanayo na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hususani kupitia ujumbe wa kawaida, *WhatsApp*, *facebook* na baruapepe. Makala yanafafanua kuwa ufutuhi kwa jamii ya Watanzania hujitokeza katika sura za ufyosi, kejeli, dhihaka na vijembe. Sura hizo za utokeaji zimehusishwa na misingi ya nadharia tatu zinazoelezea utokeaji wa ufutuhi (Nadharia ya Mkwezo, Nadharia ya Msigano na Nadharia ya Burudiko). Kuhusu dhima, makala haya yanafafanua dhima kubwa nne za ufutuhi. Nazo ni: kuwa kiungo cha kijamii, kutekeleza sanaa au fasihi ya jamii husika, kielelezo cha ujumi, na kilainishi cha maisha ya sasa.


## 1.0 Dhana ya Ufutuhi: Maana na Nadharia za Utokeaji wake

Kwa mujibu wa Ponera (2010 na 2014), ufutuhi ni mjumuiko wa hali za uchangamfu, furaha na kicheko inayotokana na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto. Kwa kawaida, maneno, matendo, au matukio hayo yenye uwezo wa kuzua hali hiyo ya ufutuhi huwasilishwa kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kisanaa kama vile kejeli, dhihaka, ufyosi, ubeuzi, tashtiti na utani. Vipengele vyote hivi, kwa mujibu wa makala haya, ni vijenzi vya ufutuhi. Vijenzi hivi kwa ujumla huwa na uwezo wa kusababisha mambo matatu ambayo ni ucheshi, kicheko, na/au furaha. Mambo haya yanafungamana kwa kiasi kikubwa. Kufungamana huko, hatimaye, kunatuleta katika hoja ya kupanua mawanda ya kushughulikia masuala yahusianayo na raha, furaha, kicheko, na ucheshi kwa kutumia istilahi ya ufutuhi. Kwa hiyo, kulingana na makala haya, mambo haya yote yanachukuliwa kuwa ni matokeo ya ufutuhi.

Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu matokeo haya matatu (ucheshi, kicheko na furaha) ili kuonesha jinsi yanavyoingiliana: Ucheshi ni hali ya kuwa

mchangamfu na mwenye furaha kwa mtu au watu wengine. Katika maisha ya kawaida (yaani, nje ya fasihi) dhana hii huhusishwa na tabia; aghalabu, tabia ambayo mtu huidhihirisha kwa muda mrefu. Maelezo haya yanatupatia hoja muhimu kuwa ucheshi hujumuisha uchangamfu, ukunjufu wa moyo, pamoja na furaha. Furaha, kwa upande wake, ni kionjo cha kisaikolojia kinachohusu hali ya ukunjufu wa moyo na bashasha ambayo aghalabu, hutokana na kuridhika — kwa moyo au akili (TUKI, 2004). Kuridhika huko mara nyingi husababishwa na mtu kutenda au kutendewa matendo, kuambiwa maneno, au kutokewa na hali ambayo inaendana na matakwa, malengo, au vionjo vyake. Furaha huweza kudhihirishwa kupitia miguno, mbinja, vicheko, vigelegele, vilio, mayowe na kurukaruka. Mtu anaweza kuwa na furaha bila kucheka na mwingine anaweza kucheka hata kama hana furaha. Msingi wa tofauti kati ya furaha na ucheshi uko katika dhana ya tabia. Hii inamaanisha kuwa furaha inaweza kuwa ni jambo linaloonekana kwa mtu katika baadhi tu ya nyakati au siku ilhali ucheshi unaweza kuonekana katika sehemu kubwa ya maisha ya mtu (isipokuwa katika baadhi tu ya nyakati awapo katika miktadha ya majonzi kama vile msibani).

Dhana ya kicheko inafasiliwa na Whipple na Calvert (2008) kuwa ni sauti itolewayo na mtu achekapo. Wanaongezea kuwa, sauti hii ni mwitikio wa kibiolojia ambao mwanadamu huutoa ili kumaanisha hali mbalimbali kama vile furaha, dharau (kubeua) au hata maumivu. Maelezo haya yanatuangazia kuwa kuna kicheko cha kuafiki, cha kukanusha, cha kubeza au kukejeli, cha kujengea au kukazia hoja, pamoja na cha kung’ong’a. Hapa pia tunadokezwa kuwapo kwa uhusiano kati ya kicheko na furaha.

Kwa hiyo basi, kimatumizi, dhana ya ufutuhi huweza kuchukuliwa kwa mitazamo mikubwa miwili: Mtazamo wa kwanza ni huo wa kuuegemeza kwenye matokeo (ya vijenzi kama vile kejeli, ubeuzi na utani). Mtazamo wa pili ni mpana zaidi ambapo ufutuhi huchukuliwa kuwa ni jumla ya hatua na mambo yote yanayounda mazingira ya kutokea kwa tabasamu, kicheko, au furaha. Mambo hayo hujumuisha mhusika mwenyewe, maneno au matendo yake, hatua za utendaji au unenaji, pamoja na mwonekano wake.

Ufutuhi ni dhana inayoweza kutokea au kufanyika kwa watu wa jamii zote. Hata hivyo, huwa kuna tofauti katika kutokea kwake kutokana na watu kutofautiana uwezo wa kuuunda au kuupokea. Tofauti za upokezi wao husababishwa na vigezo vya kihistoria, kiutamaduni, kisaikolojia na kiepistemolojia. Zaidi ni kwamba, jamii mbalimbali hapa ulimwenguni hupishana katika vipengele vya maadili, itikeli, maarifa, na ujumi. Akisisitiza kuhusu hoja hii ya tofauti, Ross (1998) ambaye anajiegemeza katika dhana ya ucheshi, anasema kuwa suala la kuwa na kionjo binafsi (cha kimaarifa na kisemantiki) ni la muhimu sana katika uibuaji wa ucheshi. Anaongeza kuwa, kionjo cha mtu hubadilika kulingana na muktadha wa kiwakati au kimahali. Hii inamaanisha kuwa ni vigumu kwa watu wawili au zaidi kufanana katika jinsi ya

kukipokea kichocheo chochote cha ufutuhi. Hali hiyo, kwa upande mwingine, itatofautisha pia kiasi cha ufutuhi (ucheshi, furaha au kicheko) atakachokipata mtu.

Baada ya maelezo hayo kuhusu maana, maelezo yanayofuata yanalenga kujibu swali la “ufutuhi humtokeaje mtu?” yaani, “ni nini hasa kinasababisha kutokea kwa hali ya ufutuhi kwa mtu au watu?” Jibu la swali hili limefungwa katika misingi ya nadharia tatu za utokeaji wa ufutuhi. Nadharia hizo ni: Nadharia ya Mkwezo, Nadharia ya Msigano na Nadharia ya Burudiko.

Nadharia ya Mkwezo ilikuwapo toka zama za Plato na Aristotle. Hata hivyo, wao hawakuitazama dhana hii kwa jicho la kinadharia, bali waliitazama kama dhana tu iliyokuwa inajitokeza katika ufafanuzi wa masuala mbalimbali. Plato, kwa mfano, ananukuliwa na Billig (2005) akiielezea kupitia dhana ya kicheko akidai kuwa watu huwacheka watu wenye uduni au wenye sura mbaya kwa sababu wao (wachekaji) hujisikia furaha kujiona kuwa wana hadhi kuliko wao (wanaochekwa). Kwa ujumla, nadharia hii inadai kuwa mtu hucheka kwa sababu ya kujiona kuwa yuko katika hadhi ya juu; na kwamba, wakati huo mtu hujikweza na kujiweka huru zaidi akiwa amejitenga na hali yoyote ya uduni (hali ya matatizo). Kutokana na msingi huo, nadharia hii hujulikana pia kama “Nadharia ya Ugandamizaji.” Kucheka hapa kunanasibishwa moja kwa moja na kutosheka au kuridhika kwa nafsi ambako, aghalabu huzaa furaha. Yaani, mtu anapocheka, hutawaliwa na raha ya aina fulani na kujiona yuko katika tabaka la pekee hata kama anazungukwa na matatizo. Punde atokapo nje ya muktadha wa kicheko chake ndipo huweza kurudi katika kuyawazia matatizo yake. Hivyo, kulingana na nadharia hii, jambo linalochochea kutokea kwa ufutuhi ni uduni unaojidhihirisha au kuonwa kwa mtu mwingine. Nadharia hii ya Mkwezo, kwa mujibu wa Provine (2000) na Morreall (1983) ambao wamenukuliwa na Billig (2005), ilidumu kwa takriban miaka elfu mbili kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Nadharia ya Msigano.

Nadharia ya Msigano, kwa mujibu wa Schuette (2010) na Billig (2005), inasisitiza kuwa ufutuhi hutokea kwa mtu mara tu mawazo yake yanapokataa kuafiki neno au jambo lililotendwa baada ya kubaini kuwa liko kinyume au tofauti na lilivyopaswa kuwa. Hivyo, madai ya msingi hapa ni kubainika kwa msigano baina ya neno au jambo lilivyo na jinsi lilivyopaswa kuwa. Kwa ujumla, nadharia hii inasisitiza kuwa, kimuundo, dhana au hali yoyote yenye uwezo wa kuzua ufutuhi lazima iwe na pande mbili zinazosigana “kwa undani” (kulingana na tafsiri au uelewa wa mpokeaji). Utokeaji wa ufutuhi kwa misingi ya nadharia hii hujikita katika utofautishaji wa dhana au hali ambazo zinaonekana kulandana kwa sura au mwonekano wa jumla; lakini, kwa undani huwa tofauti. Schuette (2010) anaongezea kuwa katika hatua ya awali, dhana hizo hukusanywa kwa pamoja katika fikra za mpokeaji kwa haraka sana. Kisha, kwa kutumia misingi ya tajiriba kuhusu hali au dhana hizo, mpokeaji huzizamia

na kubaini kutofautiana kwazo; hatimaye hujiwa na ufutuhi utendekaji wa michakato yote hii huhitaji misingi ya kisaikolojia, kihistoria, na kiutambuzi.

Nadharia ya tatu ni Burudiko. Kwa mujibu wa Scheel na Gockel (2017) na Lippit (1991), wadau wakuu wa nadharia hii ni Herbert Spencer na Sigmund Freud. Nadharia hii iliyoshika kasi mnamo nusu ya pili ya karne ya 19 inachukulia kicheko kama burudani itoayo tiba kwa aina mbalimbali za maradhi. Hii ni kwa sababu kicheko hubeba dhima ya kusukuma msongamano wa mawazo kutoka akilini na mwilini mwa mtu. Majumuisho haya yametoka katika fikra za Ben Johnson ambaye mnamo karne ya 16 aliasisi "Mkabala wa Vimiminika Vinne vya Mwili." Alifanya hivyo kupitia kazi zake maarufu za kifutuhi za *Every Man in His Humour* (1598) na *Every Man Out of His Humour* (1599). Mkabala huu unasisitiza umuhimu wa kuwapo kwa uwiano mzuri baina ya vimiminika vinne vya mwili ambavyo ni damu, nyongo nyeusi, nyongo ya njano, na uteute. Vimiminika hivi huufanya mwili pamoja na akili kuwa na afya njema, hivyo, kuuwezesha kufanya kazi zake zote kwa urahisi na ufanisi. Lakini kukiwa hakuna uwiano mzuri baina ya vimiminika hivyo, damu husababisha msongo wa mambo, hatimaye hasira. Kwa ufupi, nadharia inadai kuwa hali za raha, furaha, au kicheko ni matokeo ya utendekaji wa michakato ya uwianishaji wa vimiminika hivyo kwa kiasi cha kutosha; na kwa upande mwingine, hali za maumivu, jitimai na namna nyinginezo za kitanzia ni matokeo ya utendekaji hafifu wa michakato ya uwianishaji wa vimiminika hivyo.

Kwa kuhitimisha, maelezo ya hapo juu kuhusu nadharia za utokeaji wa ufutuhi yanatupambanulia mitazamo mikubwa miwili inayoelezea jinsi mtu anavyoweza kupatwa na ufutuhi (na hivyo kuweza kuudhihirisha). Mtazamo wa kwanza ni ule usemao kuwa ufutuhi hutokana na kuridhika kwa nafsi; kwamba, ni mdhihirisho wa jinsi mtu alivyopendezwa na vionjo alivyoviona au kuvisikia. Mtazamo wa pili unashikilia kuwa ufutuhi hutokana na aina fulani ya ubezaji, upingaji, uhojaji, au uhakiki kutokana na mtu kukumbwa na hali ya kutokukubaliana na jambo, hali, kitu au tendo fulani. Ijapokuwa tukio hili hutokea kwa haraka, huhitaji na hutegemea sana misingi ya kiutambuzi na tajiriba. Misingi hiyo ndiyo imsaidiayo mtu kupata hisia za kugongana au kupishana kwa fikra baina ya uhalisi wa uelewa wake kuhusu jambo husika dhidi ya kile kilichodhihirishwa mbele yake kuhusiana na jambo hilohilo (Kennedy na Gioia, 2007).

Kigezo cha msingi anachopaswa kuwa nacho mtu ili kukoleza mambo hayo mawili (kupata ridhiko la nafsi au akili pamoja na kuubaini unyume/msigano) ni "Hifadhi ya Maarifa." Attardo (2001), anaifasili dhana ya Hifadhi ya Maarifa kuwa ni kumbukumbu ya jumla kuhusu maarifa, ujuzi, au hali ambazo zimo katika akili ya mtu kutokana na tajiriba. Anasisitiza kuwa ili taarifa iweze kuibua ufutuhi (kicheko, ucheshi na furaha) kwa mtu, sharti pawe

na urari baina ya msimbaji (muundaji) na msimbuaji (mpokeaji). Urari huo hujengwa vema kupitia Hifadhi ya Maarifa. Katika hali ya kawaida, matini huwa haitoki katika ombwe; yaani, lazima iwe inahusiana kwa namna moja au nyingine na uzoefu fulani unaohusiana na mazingira, tabia, au matukio ya watu wa jamii husika. Kwa hiyo, mambo hayo huwa katika utambuzi wa wanajamii ambao ndio wapokeaji; na kwamba, hupaswa "kuyakumbuka." Kukumbuka huko ndiko kunakomwezesha msimbuaji kubaini kuwapo kwa ama unyume, balagha, fumbo, mchezo wa maneno, au utwezaji; na hatimaye, kuzua ufutuhi. Attardo (k.h.j.) anaendelea kubainisha sifa za "Hifadhi ya Maarifa" ambazo wapokezi wanapaswa kuwa nazo; sifa hizo ni:

a) Kuwa na utambuzi kuhusu maana ya kawaida au maana ya kikamusi;
b) Kuwa na mabunio kuhusu maana ya kipragmatiki ya tukio au hali husika;
c) Kuwa na hitimisho au mtuo;
d) Kuwa na tathmini ya kihisia kuhusu hali au tukio husika; kwa mfano, kuamua kuhusu iwapo tukio husika ni ombi au amri, sahihi au si sahihi, au zuri au baya, na;
e) Kupata ingizo jipya au rekebisho la fikra kutokana na tathmini iliyofanywa (kur. 49-53).

Maelezo hayo yanatuthibitishia kwamba matendo ya uundaji na upokeaji wa ufutuhi hushirikisha maarifa na idili za kijamii. Hii ni kwa sababu matendo yote hayo mawili (uundaji na upokezi wake) huhusisha hatua ya juu ya kuchanganua na kutafsiri matini za kiuneni, kimatendo, au kimaandishi. Kwa hiyo, ili ufanisi utokee, ni lazima pawe na matumizi ya milango mingi ya fahamu itakayoweza kuvimulika, kuvihuisha na kuvihusisha vipengele vya kijiografia, kihistoria, kisaikolojia na kiutamaduni. Hali hii inapaswa iwe ya kiwango sawa au kinachokaribiana miongoni mwa wanajamii au watu (kuanzia wawili na kuendelea) wanaofanyiana ufutuhi. Kinyume chake, dhana ya kudhihirika kwa ufutuhi itapwaya na kukosa mashiko.

## 2.0 Sura za Ufutuhi Unaojitokeza katika Jamii za Watanzania

Sehemu hii inajadili sura mbalimbali za jinsi ufutuhi unavyojitokeza katika jamii za Watanzania. Sura hizo zinadhihirishwa kupitia data 23 za ujumbe zilizokusanywa kupitia akaunti za mitandao ya ki-TEHAMA (ujumbe wa kawaida, *WhatsAp*, *facebook* na baruapepe) za mwandishi kutoka kwa marafiki na wafanyakazi wenza. Ufuatao ni ujumbe wenyewe (kwenye mabano ni tarehe za kupokelewa kwa ujumbe husika). Baada ya udondozi wa ujumbe huo, umefuatia ufafanuzi:

a) Binti aliyetoweka kijijini kwao alirejea nyumbani baada ya kutoweka kwa miaka kumi. Mahojiano yakawa hivi:

Baba: "Wee mtoto, ulipotelea wapi, hivi unajua kuwa ulimtesa sana mama yako?"

Binti: "Nilikuwa huko Marekani nafanya kazi ya UMALAYA."

Baba: "Mshenzi mkubwa wee! Umetutia aibu wazazi wako. Toka hapa na usikanyage tena hapa!"

Binti: "Sawa baba, nitaondoka; ila kabla sijaondoka, ningependa kuwaambia kuwa nimewanunulia nyumba ya kisasa mjini, nimewawekea milioni 75 katika akaunti ya benki niliyowafungulia, na gari nililokuja nalo ni la kwako."

Baba: (*akiongea kwa sauti ya upole*) "Hivi ulisema unafanya kazi gani vile huko?"

Binti: "Umalaya."

Baba: "Anhaaa! Mi' nilisikia 'UYAYA'. Pole na kazi mama! Karibu ndani mwanangu" (Desemba 5, 2012).

b) Kwanza, uuangalie, kisha polepole uuweke mdomoni, uunyonye kidogo huku ukiupaka mate ili unyooke vizuri! Utoe vizuri, kisha ushikeshike hapo mbele ili uendelee kunyooka. Kisha taratibu upeleke tunduni. Unaweza kufumba jicho moja ili kuongeza umahiri. HIYO NDIYO NJIA RAHISI YA KUINGIZA UZI KWENYE SINDANO! Sasa unashangaa nini? Kwani we' ulikuwa unadhani nini? (Desemba 8, 2012).

c) Jamaa alikatika mkono mmoja. Baada ya kuona maisha yanazidi kuwa magumu, akapanda ghorofani ili ajitupe chini. Kabla hajajitupa, akamwona mtu asiye na mkono hata mmoja akirukaruka. Akamuuliza: "Mbona unarukaruka kwa furaha wakati huna mikono yote?" Jamaa akamjibu: "Furaha wapi? Huko mgongoni kunaniwasha, nashindwa kujikuna!" ...Jamani, usijione kuwa una shida zaidi; kuna watu wakikueleza matatizo yao, utatamani utembee uchi! (Desemba 21, 2012).

d) Swali letu la kipimajoto kwa leo linasema hivi: "Kutokana na tabia ya makonda wa daladala kuwapitiliza wateja wao vituo kwa kutosikia kwa sababu hutoa vichwa vyao nje pindi wanapoambiwa

'washushe'; Je, kuna haja ya makonda kuhamishiwa masikio makalioni, maana ndiyo yanayobakia ndani wakati wote? Andika "N" kama unakubali na "H" kama unakataa (Desemba 15, 2012).

e) Ninavyoitamani, ninavyoithamini, ninavyoitaka, ninavyoipenda, ninavyoililia, ninavyoi-*miss*, nilivyokuwa na hamu nayo na hivi sijaipata kwa muda mrefu. *Wallahi*, nikiipata nitaisugua mpaka ichubuke... Unacheka nini? MIE NAZUNGUMZIA VOCHA YA SH. 10,000/=; maana si' kila siku natumia ya 'jero' au ya 'buku' tu! Au we' ulifikiria nini?! (Desemba 15, 2012).

f) Jamaa alifumaniwa, akakimbilia kwenye daladala akiwa uchi... Konda akawa anamuangalia sana yule jamaa. Baada ya kuona anaangaliwa sana, jamaa akamuuliza konda: "Sasa unanishangaa nini...?". Konda akamjibu: "Wala sishangai uchi wako, najiuliza nauli umeweka wapi?!" (Januari 9, 2013).

g) Kuna dereva *tax* mmoja alimpakia mzungu anayejua Kiswahili. Wakawa wanapiga *story*; sasa dereva akatokwa na ushuzi wa kimyakimya. Akawa anamuangalia Mzungu; na akamuuliza swali la kumpoteza: "Unaionaje hali ya hewa ya huku kwetu Tanzania?" Mzungu akajibu: "Kama itaendelea hivihivi, muda si mrefu, INAWEZA KUNYESHA MVUA YA MAVI (Januari 12, 2013).

h) Jamaa mmoja alikuwa anasumbuliwa na panya; akaamua kuwatega kwa sumu kwenye nyama ya nguruwe. Kesho yake asubuhi alipoenda pale alipotega, akakuta karatasi imeandikwa: "TUWEKEE NA SAMAKI, SISI WENGINE NI WAISLAMU" (Januari 13, 2013).

i) Wangoni kwa *swaga*, yaani we' acha tu! Dar es Salaam wanaita 'KU-DALESALAMA'; na Shirati wanaita 'KU-SHILATI'... Je, kwa kufuata utaratibu wao huo, unadhani MARANGU wataiitaje? Nisaidie rafiki yangu (Januari 18, 2013).

j) Ukiona mvua inanyesha usinitumie *sms*, maana zinakuja zikiwa zimelowa hewani; mpaka nizianike juani au kwenye moto ndipo zisomeke vizuri. Kukiwa na joto kali *sms* zinakuja zikitoa jasho na harufu mbaya. Kukiwa na baridi, zinakuja zikiwa zinatetemeka. Pia, kukiwa na upepo, zinakuja zikiwa hazijakamilika sababu

maneno mengine yanapeperushwa na upepo hewani. Zingatia hali ya hewa kabla haujatuma *sms* yako (Januari 26, 2013).

k) Baba: "Mbona leo umeamka alfajiri sana?"
Mtoto: "Namuwahi mwalimu wa bagia!"
Baba: "Badala ya kuwahi masomo, unawahi bagia?"
Mtoto: "Elimu haina mwisho! Ila bagia huwa zinaisha saa 4 tu baba! (Februari 3, 2013).

l) Daktari bingwa wa magonjwa ya moyo alifariki. Kwa heshima, wakaamua kumchongea jeneza lenye umbo la moyo. Wakati wa kuaga mwili wa marehemu, daktari mmoja alikuwa anacheka sana. Padri akamuuliza: "Mbona unacheka wakati tupo msibani? Au unafurahia mwenzako kufa?" Yule daktari akajibu: "Hapana Padri! Nilikuwa nafikiria tu na kujiuliza kuwa nikifa nitachongewa jeneza la umbo gani? Maana mimi ni daktari bingwa wa kutahiri" (Februari 9, 2013).

m) "*Hallow... Hallow*...! Ukivua niambie! Nina hamu sana... We' vua tu usiogope kitu...! Yaani, sijaonja hiyo kitu kwa muda mrefu sana... Hivyo, ukivua tu, nitaarifu..." MTEJA WA SAMAKI ALISIKIKA AKIMHIMIZA MVUVI MASHUHURI WA SAMAKI KULE ZIWANI. Acha kuwa na hisia za mbaaali! (Februari 10, 2013).

n) Dada alikuwa anatoka kuoga akiwa na kanga moja tu; akasikia hodi. Baada ya kufungua mlango akakuta kumbe ni John, jirani yake wa siku nyingi ambaye ni kipofu. Akamkaribisha ndani, akakaa. Naye akavua ile kanga na kubakia uchi; kisha akaendelea kujipodoa huku akimsemesha John.

Dada: "Vipi John mbona umepotea sana? Yaani, huonekani siku hizi!"
John: "Aah, hapa kati nilienda India kufanyiwa operesheni ya macho. Namshukuru Mungu, kwa sababu sasa hivi naona vizuri kabisaaa...! "
Unajua kilichotokea? Nirushie vocha nikumalizie *story* (Februari 11, 2013).

o) Mbwa koko wawili walikuwa wanasaka chakula jalalani. Mara, likapita *landrover* la FFU; na ndani yake mlikuwa na mbwa wa polisi. Mbwa koko mmoja akaangalia kwa uchungu kisha

akamwambia mwenzake: "Unaona wenzetu waliosoma waleee, wanaenda kazini! Sisi tunahangaika tu majalalani." (Februari 28, 2013).

p) Bahili mmoja alinunua mbuzi; akampatia mkewe na kumwambia: “Nyama nusu ipike pilau na nyingine iweke kwenye *freezer*; kichwa fanya supu na miguu fanya mchemsho. Na ngozi usiitupe, tutafanya jamvi. Pembe zake tutafanya mapambo sebuleni. Utumbo pika na ndizi; na mifupa tutawauzia wenye mbwa. Kinyesi ukihifadhi vizuri kwa ajili ya mbolea ya bustani.” Mkewe akauliza: “Je, hutapenda sauti ya huyu mbuzi tufanye iwe *ringtone* ya simu yako? (Februari 19, 2013).

r) Mume: “Hello *baby*!”
Mke: “Hello *sweetie*!”
Mume: “Nitachelewa kurudi leo”
Mke: “N’shajua, uko kwa vijana-jike vyako; wewe ni malaya sana. Sijui hata ilikuaje ukanioa. Nakuchukia kama nini! Yaani, sikupendi! sikupendi!”
Mume: “Niko BENKI hapa”
Mke: “Anhaaa! Ulijuaje kama sina hela! Nitolee laki moja *baby*.
Nakupenda sana kuliko roho yangu; nakutengea maji ya kuoga *sweety*. Usisahau hizo pesa ninunulie na *chips* kuku! Mmwaa!”
Mume: “Ni BENKI YA KUCHANGIA DAMU.”
Mke: “Nyoooo...! Waambie wakutoe yote!" (Septemba 16, 2012).

s) Kijana mmoja alikuwa anafagia ndani ya ndege. Kwa bahati nzuri, akaokota kitabu chenye kurasa nne zilizosomeka hivi:
Ukurasa wa 1: Ukitaka kuwasha ndege, bonyeza kitufe chekundu. Akafanya hivyo. Ndege ikawaka.
Ukurasa wa 2: Ili itembee, bonyeza kitufe cha njano. Akabonyeza; ikatembea.

Ukurasa wa 3: Ili ipae, bonyeza cha bluu. Akabonyeza; na ndege ikapaa. Akawa akijisemea kimoyomoyo: “Wanaosomea kuendesha ndege kwa miaka kibaaao ni wajinga sana! Mimi nimeishia darasa la nne tu lakini nimeweza kupaisha ndege ndani ya dakika moja...”
Ukurasa wa 4: Paliandikwa: “UKITAKA NDEGE ITUE, FIKA

CHUONI KWETU KWA MAFUNZO ZAIDI. Kijana akapoteza fahamu (Machi 11, 2013).

t) Bibi mmoja wa MTWARA alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa tumbo kwa miaka mingi. Majuzi alipelekwa hospitalini. Daktari alipompima, akamwambia: "TUMBO LAKO LIMEJAA GESI; inatakiwa ufanyiwe upasuaji." Bibi kusikia vile, ghafla akakurupuka mbio huku akipiga mayowe “Haiwezekani! Hii gesi yangu natafuta mwekezaji mimi mwenyewe! Hii haipelekwi Dar es Salaam ng'o! Kwa kweli Mungu amewajalia wana-Mtwara, wana gesi baharini hadi matumboni mwao!” (Februari 25, 2013).

u) Boti ya Azam *Marine*, ile mpya, iliyoanza safari yake ya kwenda Zanzibar ikitokea Dar es Salaam asubuhi ya leo; iliyopakia abiria wasiopungua 450 na mizigo ipatayo tani 13, imefika salama bandarini Zanzibar... Sasa unatoa macho ya nini? Sio kila zikizama nd’o tuambiane; hata zikifika salama tujulishane jamani! (Machi 4, 2013).

v) Mlevi mmoja alipita karibu na msikiti, akaona Waislamu wananawa maji ili kutia “UDHU.” Akawaangalia tu kisha akaenda zake. Aliporudi, akawakuta wamefunga swala; akasema: "Mi’ nilijua tu, kwa mchezo ule wa kuchezea-chezea maji, lazima mtaona baridi tu!". Asalaam aleykum! (Machi 9, 2013).

w) Baba alimuuliza mtoto: “Unamjua J.K. Nyerere?”
Mtoto: “Simjui”

BABA: “Pumbavu; kuwa makini na shule.”

Mtoto naye akamuuliza baba’ke: “Unamjua Mzee *Big*?”

BABA: “Simjui”

MTOTO: “Pumbavu; kuwa makini na mkeo.”

Baada ya jibu hili, yule BABA akazimia pale pale! (Machi 17, 2013).

y) Mtalii mmoja wa Kizungu alikuwa anasafiri katika mtumbwi na mwenyeji wake katika mto Rufiji. Wakiwa humo, yule mtalii akamuuliza kijana:

> *"Do you know Biology, Psychology* and *Physiology*?
>
> Kijana akajibu: "*No*."
>
> Mtalii akamwambia kwa dharau: *"What the hell do you know on the face of this earth? You will die of illiteracy!* (Ni nini sasa ukijuacho hapa duniani? Utakufa kwa ujinga wako).
>
> Baada ya muda kidogo, mtumbwi ukaanza kuzama. Mtalii akaanza kuhangaika; kijana alipoona vile akamuuliza:
>
> *"Do you know 'swimmiology' and 'escapology' from 'crocodiology'*? (akikusudia kumuuliza, unajua kuogelea na jinsi ya kujiokoa na mamba?)
>
> Mtalii akajibu: "*No"*. Kijana akamwambia:
>
> "*What the hell do you know on the face of this earth? You will 'dieology'; and 'crocodiology' will eat your 'bodyology' because of your bad 'mouthology'*!!" (akikusudia kusema, ni nini sasa ukijuacho hapa duniani? Utakufa; na mamba wataula mwili wako kwa sababu ya domo lako baya). ...Ukiujua huu, mwenzio anaujua uleee! (Machi 21, 2013).

Baada ya kuona data hizi, ufuatao ni mjadala wa sura mbalimbali ambazo kwazo ufutuhi hujitokeza na kujengwa. Kwenye mjadala huu, ujumbe huo utarejelewa kama "tukio" au "matukio." Kabla ya kuanza mjadala, hapa chini kuna jedwali linaloonesha muhtasari wa uhusiano kati ya matukio ya kifutuhi na mitazamo mikubwa miwili ya nadharia za utokeaji wa ufutuhi. Pia, jedwali linaonesha kijenzi kilichojichomoza kuliunda tukio husika. Vijenzi hivyo, kama vilivyodokezwa hapo juu, ni kejeli, dhihaka, kijembe na ufyosi. Vijenzi hivi vinatumiwa humu kwa kuzingatia maana zinazoelezwa na Ponera (2014) kuwa, msingi wa kejeli hukitwa katika unyume wa mambo; dhihaka hukitwa katika kufanyiana mzaha; na kijembe hukitwa katika kusimbiana na kusimbua mafumbo. Kwa upande wa ufyosi, msingi wake huwekwa kwenye matusi, hususani matusi yanayojielekeza katika majina ya sehemu za siri za mwanadamu pamoja na mambo yanayofanywa na sehemu hizo.

**Jedwali la Muhtasari wa Uhusiano kati ya Matukio ya kifutuhi na Nadharia za Utokeaji wa Ufutuhi; pamoja na Vijenzi vyake***:*

| **Tukio** | **Uhusiano wake na Nadharia za Utokeaji wa Ufutuhi** | **Kijenzi** |
|---|---|---|
| a. | Msigano | Kejeli |
| b. | Msigano | Ufyosi |
| c. | Msigano | Dhihaka |
| d. | Msigano | Ufyosi |
| e. | Msigano | Ufyosi |
| f. | Msigano | Ufyosi |
| g. | Msigano | Dhihaka |
| h. | Msigano | Dhihaka |
| i. | Msigano | Kijembe |
| j. | Ridhiko la nafsi | Dhihaka |
| k. | Msigano | Dhihaka |
| l. | Ridhiko la nafsi | Dhihaka |
| m. | Msigano | Ufyosi |
| n. | Msigano | Dhihaka |
| o. | Msigano | Kejeli |
| p. | Ridhiko la nafsi | Kejeli |
| r. | Msigano | Kejeli |
| s. | Msigano | Dhihaka |
| t. | Msigano | Dhihaka |
| u. | Msigano | Dhihaka |
| v. | Msigano | Dhihaka |
| w. | Ridhiko la nafsi | Fumbo |
| y | Ridhiko la nafsi | Kejeli |

Data zote zilizobainishwa hapo juu zinaafikiana na misingi ya nadharia tatu zilizodokezwa hapo juu. Sehemu kubwa ya matukio haya imejengwa katika hali ya msigano. Hii ni kutokana na kudokeza mambo kwa namna ya unyume. Ufutuhi wa matukio machache (matukio "**j**", "**l**", "**p**", "**v**" na "**w**") umejengwa na kuwapo kwa ridhiko la nafsi na akili kutokana na msisimko au mnato unaotokana na aina ya mada inayozungumziwa, uchaguzi wa maneno pamoja na mpangilio wa maneno au tungo. Kwa hiyo, makala haya yanachukulia kuwa, kutokana na matukio haya yote kuafikiana na misingi ya kinadharia, ni wazi kuwa yana uwezo mkubwa wa kuzua ufutuhi (ama kicheko, furaha, au hali ya uchangamfu na bashasha). Suala la kuwa au kutokuwa na uwezo wa kuibua

ufutuhi kwa mpokeaji pamoja na kiasi cha ufutuhi utakaomtokea hutegemea kiasi cha Hifadhi ya Maarifa aliyonayo mpokeaji kuhusu tukio husika. Mpokeaji anapaswa kuwa na kiasi cha kutosha cha hifadhi (kwa kukumbuka au kufuatilia) ya matukio yaliyosawiriwa katika matukio husika ndipo ataweza kubaini mnato au msigano unaokusudiwa; hatimaye, kuwa na uwezekano wa kupatwa na ufutuhi.

Kuhusu vijenzi vinavyoyaunda matukio haya, uchanganuzi wa jedwali la hapo juu unaonesha kuwa kuna mtawanyo mzuri wa matumizi ya vijenzi vya kejeli, dhihaka, vijembe na ufyosi katika kuunda matukio ya kifutuhi katika jamii za Watanzania. Hata hivyo, kijenzi cha ufyosi, hususani unaohusiana na masuala ya ngono kinaonekana kutamalaki. Kwa kuhitimisha kuhusu sura za ufutuhi wa jamii za Watanzania, imedhihirika kupitia data za hapo juu kuwa Watanzania huudhihirisha ufutuhi wao katika sura za ufyosi, kejeli, dhihaka na vijembe.

## 3.0 Dhima za Ufutuhi kwa Jamii ya Watanzania

Sehemu hii inajadili dhima za ufutuhi kwa jamii ya Watanzania. Dhima hizo zinajadiliwa kwa kuzingatia mifano kutoka kwenye data zilizotumiwa na makala haya. Kutokana na data hizo, inadhihirika kuwa ufutuhi una dhima kuu nne katika jamii ya Watanzania. Dhima hizo ni: kuwa kiungo cha kijamii, kutekeleza sanaa au fasihi ya jamii husika, kielelezo cha ujumi, na kilainishi cha maisha ya sasa. Ufuatao ni mjadala wa dhima hizo:

### 3.1 Kuiunganisha Jamii

Ufutuhi, kama asemavyo Bakhtin (1984), ni kitu muhimu cha kijamii ambacho huunganisha sanaa na maisha. Mwanadamu apatapo tu ufahamu wa kiakili, hutumia muda wake mwingi katika kuhakikisha kuwa anakuwa na "maisha mazuri." Kwa kiasi kikubwa, juhudi hizo huzifanya kwa kutumia sanaa. Miongoni mwa nyenzo za msingi azitumiazo katika shughuli hizo za kisanaa ni lugha. Kila lugha ina nyenzo zinazotumika kama misimbo ya kuzulia ufutuhi. Misimbo hiyo hudhihirishwa kupitia uneni, ishara mbalimbali za viungo vya mwili, lugha-uso, pamoja na matendo. Imekwisha kudokezwa hapo juu (katika sehemu iliyofafanua suala la Hifadhi ya Maarifa) kwamba matukio yatumikayo kuundia ufutuhi hutoka katika jamii, na hutokana na ama wanajamii wenyewe, au tabia zao au matendo yao. Vilevile, huundwa ili kukidhi mahitaji ya wanajamii wenyewe. Ukweli huu ndio unaoufanya ufutuhi uchukuliwe kuwa unajitokeza kama tukio au hali ya kijamii. Katika kutekeleza dhima hii, ufutuhi huweza kutumika kama nyenzo ya mawasiliano, tukio la kielimu, pamoja na pedagojia ya kuendeshea mambo mbalimbali.

### 3.1.1 Ufutuhi kama Nyenzo ya Mawasiliano ya Kila Siku

Haiman (1998) anafafanua kuwa, kwa kawaida, binadamu hutumia lugha za namna kuu mbili katika mawasiliano yake ya kila siku, yaani lugha ya wazi na lugha isiyo ya wazi. Lugha ya wazi ni ile itumiayo maneno yenye maana ya moja kwa moja; na ile isiyo ya wazi hutumia msamiati na misimbo ya kifasihi ambayo, aghalabu, haiwi na maana ya moja kwa moja. Ufafanuzi wake unahitimisha kuwa, lugha isiyo ya wazi ndiyo ambayo huitumia zaidi kwa madhumuni ya kufanikisha mawasiliano yake. Hii ni kwa sababu huweza kutumiwa peke yake (bila kuichanganya na lugha ya wazi) na wakati mwingine kwa kuichanganya. Imeelezwa pia kuwa sehemu kubwa ya mazungumzo na mawasiliano mengine kama vile ya kutoa rai, kukemea, kuomba, na kuonya hufanywa kwa kutumia lugha ambayo hunyunyiziwa misimbo na vionjo vya kifasihi na kwamba, mawasiliano yanayoendeshwa kwa lugha ya moja kwa moja peke yake hufanyika mara chache. Maoni kama hayo pia yametolewa na Palmer (1994) ambaye anaongezea kwa kusema kuwa namna hiyo ya lugha pia hujulikana kama "lugha ya kifutuhi." Maoni haya ya Palmer yanadhihirisha moja kwa moja kuwa ufutuhi ni sanaa inayotumia lugha isiyo ya moja kwa moja.

Watanzania, kama walivyo watu wa jamii nyingine, huutumia ufutuhi kwa ajili ya mawasiliano yao ya kila siku, iwe katika miktadha kama vile ya maongezi ya ana kwa ana au kwa simu, kuombana na kukaripiana. Zaidi, huutumia kuakisi matukio yatokeayo kila siku katika jamii zao. Utumiwapo kimawasiliano, ufutuhi huo hubinywa na mipaka ya kimahusiano kwa kuzingatia vigezo vya umri, vyeo vya kikazi, au uhusiano wa kifamilia au kiukoo. Mbali ya mifano ya jinsi Watanzania watumiavyo ufutuhi katika mawasiliano yao ya ana kwa ana, mwelekeo wa kiufutuhi pia huonekana katika misemo ambayo baadhi ya Watanzania huiandika katika sehemu kama vile za biashara na vyombo vya usafiri. Zaidi ya hayo, kupitia maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika TEHAMA, siku hizi ufutuhi hujitokeza zaidi katika mawasiliano wayafanyayo kupitia nyenzo za ki-TEHAMA kama vile simu za kawaida, na mitandao ya *Facebook*, *Whatsapp*, *Baruapepe*, *Instagram* na *Viber*. Sehemu kubwa ya Watanzania hujihusisha na kupokea au kutuma ujumbe wenye ufutuhi. Hii husababisha mzunguko mkubwa wa ujumbe wenye ufutuhi ndani yake ambao watu wanapeperushiana kupitia nyenzo hizo (rejea data 23 za ujumbe za hapo juu). Kwa kawaida, ujumbe huo hutumwa kwa kuzingatia mipaka ya kimahusiano; yaani huwa hazitumwi kwa kila mtu. Hii ni kwa sababu sehemu ya ufutuhi huo huwa imefungwa ndani ya mafumbo, kejeli, ung'ong'aji, tashtiti, ufyosi na utani wenye hali ya matusi ndani yake. Kwa hiyo, watu wenye kuelewana, kuendana na kuhusiana ndio huhusika katika kutumiana ujumbe

huo wenye mwelekeo wa kifutuhi. Kupitia ujumbe huo wenye mwelekeo wa kiufutuhi watu hufunzana, huburudishana, huonyana, na kukosoana.

Kwa kuzingatia kuwa ujumbe huo umekuwa ukizunguka miongoni mwa Watanzania, na kwamba, yumkini, hutungwa na watu wa sehemu, hadhi, na itikadi mbalimbali, inahalisi hapa kusema kuwa hii ni ithibati maridhawa ya mwelekeo wa Watanzania katika jambo hili la matumizi ya ufutuhi ndani ya jamii. Ndani ya ujumbe huo, tunaweza kuona watu wanavyotwezana, wanavyo-tukanana, wanavyooneshana viashiria vya ubwege, na wanavyodhihakiana. Mathalani, inaonekana kuwa sehemu kubwa ya mifano hii inajielekeza katika hali ya utusiutusi unaotokana na kushambuliwa kwa majina, matendo, na matokeo yanayohusiana na eneo la katikati la mwanadamu ambalo lina sehemu za siri.

Zaidi ya hayo, mifano hiyo inatuyakinishia ukweli kuhusu umuhimu wa mshirika wa kufanyiana ufutuhi kuwa na "Hifadhi ya Maarifa" kama ambavyo imekwisha kudokezwa hapo juu. Ni dhahiri kwamba, ili kuufaidi ufutuhi uliomo katika mifano hiyo, ni lazima kuwa na kiasi cha kutosha cha utambuzi wa jambo linalokejeliwa au kufanyiwa ufyosi. Kwa mfano, ni vigumu kwa mtu kujiwa na ufutuhi katika mifano ya tukio "**t**" na "**u**" ya hapo juu bila kuwa na maarifa kuhusu mambo yanayozungumziwa. Tarehe za kupokewa kwa ujumbe huo pamoja na maudhui yake zinamtaka kwanza mtu akumbuke matukio makubwa mawili: La kwanza (lililomo katika tukio "**t**") linahusu maandamano yaliyoambatana na tafrani kadhaa ambayo yalifanywa na watu wa mikoa ya Lindi na Mtwara mwanzoni mwa mwaka 2013 kudai nishati ya gesi iliyogundulika huko isisafirishwe kwenda nje ya mikoa hiyo. La pili (tukio "**u**") linarejelea matukio ya ajali mbili za meli za *M.V. Spice Islander I* na *M.V. Skagit* zilizotokea katika mkondo wa Nungwi, katika Bahari ya Hindi, zikiachana kwa kipindi kisichozidi miezi kumi. Ya kwanza ilitokea Septemba 10, 2011 huku watu takribani 1,500 wakiripotiwa kupoteza maisha; na nyingine ilitokea Julai 12, 2012 na kuua zaidi ya watu 150. Kwa hiyo, ufutuhi uliomo humo unachimbuka katika taharuki impatayo mtu kutokana na kuwa na maarifa kuhusu tanzia hizo.

### 3.1.2 Ufutuhi kama Jambo la Kielimu

Ufutuhi pia hujidhihirisha katika jamii za Watanzania kama jambo la kielimu. Licha ya ukweli kuwa tukio lolote la kifutuhi huwa na sura au pande mbili za mtendaji na mlengwa ambazo pia huwa na athari tofauti (chanya na hasi), kwa jicho la kielimu, matukio hayo hubeba namna fulani ya ujumbe (jambo la kujifunza) katika namna ya ufiche. Ujumbe huo huweza kuwa na lengo la kufundisha, kukosoa, kukumbusha, au kuonya. Kwa hiyo, licha ya maadili yabebwayo na tukio au hali hiyo, hata utafutaji na ufumbuzi wa maana na maadili ya tukio husika pia ni namna ya kupata elimu.

Kwa kurejelea mifano ya ujumbe uliodondolewa hapo juu, licha ya kejeli, vijembe, na mafumbo yaliyomo kuleta hali za kuumiza, kuhuzunisha na kufadhaisha, lakini katika upande wake wa pili ujumbe huo unatubainishia maadili muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na wanajamii. Mathalani, tunaadilishwa kuhusu athari za ujivuni katika matukio "**w**" na "**y**". Tukio "**y**" ambalo linawahusu wahusika wawili wenye maarifa na ujuzi katika mambo tofauti linatuonya kuhusu kujikweza na kujivuna. Zaidi, linatufundisha kwamba, tunapaswa kuwathamini watu wengine licha ya kuonekana kuwa duni, kwani wana jambo wanalolijua na lenye manufaa katika ustawi na uhai wa mtu mwingine. Mafunzo yote haya yamefunikwa na kejeli na upindishwaji (kama vile wa maneno *swimmiology*, *escapology*, *crocodiology*, na *mouthology*) wenye uwezo wa kumzulia ufutuhi mpokeaji mwenye hifadhi ya maarifa.

Vilevile, tunafundishwa kuhusu athari za ujinga katika matukio ya "**r**", "**s**" na "**v**". Tukio "**s**", mathalani, kwa sura ya jumla linabebwa na taharuki nzito inayompata kijana aliyefanikiwa kuiwasha na kuirusha ndege kwa bahati, kisha anabaini kuwa hana ujuzi wa kuifanya itue salama. Ni taharuki hii ndiyo inayoweza kumjengea mpokeaji msigano (wa hali ya kijana kurusha ndege kwa kusoma tu katika kipeperushi dhidi ya uhalisi wa kitakachotokea baada ya kufanikiwa kuwa angani kinasibu). Kwa jicho la ndani, tukio hili linadokeza hatari ya ujinga na papara.

### 3.1.3 Ufutuhi kama Pedagojia ya Kuendeshea Mijumuiko ya Kijamii

Thamani ya ufutuhi inajitokeza pia wakati wa mijumuiko ya kijamii inayotokea katika jamii nyingi hapa Tanzania. Mijumuiko hiyo huhusu shughuli kama vile ibada, mazishi, shughuli za kitaaluma (ufundishaji), matamasha ya michezo, mikutano (ya kisiasa, kidini, au kitaaluma), pamoja na sherehe (kama vile za jando, unyago, harusi, mavuno, au kupata mtoto). Palmer (1994), Janik (1998) na Limbe (2012) wanasisitiza kuhusu kuenea kwa matumizi ya wahusika wa kibwege katika jamii mbalimbali ulimwenguni. Palmer (1994), kwa upande wake, anahusianisha ufutuhi na kuwapo kwa michezo ya kibwege. Hali hiyo ya kuwapo kwa wahusika wa kibwege, ijapokuwa ni kwa viwango tofauti vya ubwege, ipo pia katika jamii za Watanzania. Kwa mujibu wa Janik (1998) na Limbe (2012), wahusika wa kibwege, aghalabu, hujibaradhulisha katika maneno na/au matendo yao. Baadhi ya sifa za ubwege (fasihi ya kibwege) ni msuko wa matukio usiofuatana kimantiki, kuhusisha mazungumzo ya kubwabwaja na vitendo visivyoelewekaeleweka (visivyo na mantiki iliyo bayana) na kutumia mtindo wa kindoto.

Miongoni mwa mazingira mashuhuri katika matumizi ya ubwege ni yale ya mazishi (uendeshwaji wa tukio zima la msiba kama vile utoaji wa taarifa za kifo [kama kilitokea mbali na anapotakiwa kuzikwa], uandaaji wa chakula, uandaaji wa kaburi, jinsi ya kuwaliwaza wafiwa, na hatimaye maziko

yenyewe). Kwa mfano, hatua muhimu za msiba husimamiwa na kuendeshwa na kundi maalumu la watu kutoka katika kabila au ukoo mwingine ulio katika mahusiano ya kiutani na familia iliyofikwa na msiba. Uendeshaji huo huambatana na matendo na kauli zenye kutweza, kukejeli, na kudhihaki. Aghalabu, matendo na kauli hizo huelekezwa katika mwonekano au tabia za marehemu. Pamoja na kujibaradhulisha huko, watani hao huhakikisha mambo yote lazima yaende vema ili kufika katika kilele cha shughuli. Hii ni kwa sababu, namna yoyote ya anguko au kushindwa kutakakotokea katika familia au ukoo itawafedhehesha pia familia au ukoo huo wa watani. Pia, matendo ya kibwege yenye uwezo wa kuzua ufutuhi hujidhihirisha katika michezo kama vile bao kwa watu wazima; na mpira wa miguu na drafti kwa vijana na watu wa makamo. Matumizi ya majigambo, ufyosi na tashtiti katika mazingira haya ya michezo huwa ni jambo la kawaida hata kusababisha baadhi ya wanaofuatilia kucheka, kufurahi au kutabasamu.

Muktadha mwingine utumiao vionjo vya kifutuhi katika kuendeshea shughuli zinazowahusisha watu wengi kwa pamoja ni ule wa ufundishaji. Wagner (2007: 15-18), kupitia uzoefu wake katika kazi za ualimu na uhubiri wa dini, anasisitiza kuwa ufundishaji huhitaji kunyunyiziwa vionjo vya kifutuhi bila kujali aina ya somo lifundishwalo wala aina ya wanafunzi. Anaongeza kuwa hadhira yake huelewa zaidi pale anapoipa fursa ya kucheka kuliko anapowanyima kabisa. Kwa hiyo, anahitimisha Wagner (k.h.j.) huku akiungwa mkono na Geybels na Van Herrck (2011), ni muhimu sana kupenyeza vionjo vya kiucheshi na kicheko katika wasilisho lolote. Kwa hiyo, kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa licha ya ufutuhi kubeba maadili mbalimbali, wenyewe pia huweza kujitokeza kama umbo la kipedagojia. Yaani, kwalo, mambo mengine hufanyika kwa ufanisi zaidi.

### 3.2 Kutekeleza Sanaa Jamii

Kinachorejelewa zaidi hapa katika kuuchukulia ufutuhi kama jambo la kisanaa ni ufundi wa kisanaa unaoshuhudiwa katika matukio yatendwayo na watu au jamii tofauti. Ufundi huo hujitokeza katika kuteua mada ya kuundia tukio, kuichagulia maneno na ruwaza maalum ili kujenga mnato na/au msigano, na kwa hakika, tofauti hizo ndizo zinazoleta raha ya kisanaa katika hali au matukio hayo.

Watanzania huvitumia vijenzi mbalimbali vya ufutuhi huku kukiwa na tofauti katika kuunda kejeli, mafumbo, tashtiti, dhihaka na ufyosi kati ya mtu mmoja na mwingine au jamii moja na nyingine. Tofauti hizo huweza kutokana na mila, desturi, maadili ya jamii, pamoja na vionjo vinavyotokana na uwezo binafsi wa mtu. Haya yote huweza kudhihirika katika kazi mbalimbali za fasihi nenwa (mazungumzo, majigambo, masimulizi, misemo, na nyimbo) na fasihi andishi. Ufutuhi wa kiuneni hufanywa ama ana kwa ana au kupitia vituo vya

runinga na redio. Ross (1998), Wamitila (2010) na Senkoro (2011) wanadokeza kuwa mambo yanayoweza kuzingatiwa katika kuuibua ufutuhi katika tanzu za kiuneni ni pamoja na kuwapo kwa utata, mwingiliano matini, mwigobezi, majazi, ufumbaji, dhihaka, kinaya, lugha-uso, vipashio vya fonolojia arudhi, pamoja na tauria (vichezea maneno na vitanza ndimi). Katika fasihi andishi, ufutuhi umefanikiwa kusimama kama mbinu inayojitosheleza ya kufikishia ujumbe kwa hadhira.

Matukio yaliyodondolewa hapo juu yamebeba sifa hizo za ufasihi kwa kuwa yameundwa kwa kutumia vijenzi vilivyodokezwa (kama vile dhihaka, kejeli, na mafumbo), hatimaye kuwa na uwezo wa kuzua ufutuhi kwa mpokeaji. Mifano ya wazi zadi inaweza kuonekana katika matukio "**m"** na "**n**". Usanaa wa tukio "**m**" umejifunga katika fumbo. Inaelezwa awali kuwa jeneza la daktari bingwa wa moyo limeundwa kwa kusadifu umbo la "moyo." Mpokeaji anapotumia vema hifadhi ya maarifa kuhusu kiungo kinachohusika na tendo la "kutahiri" ndipo atakapoweza kufumbua fumbo la jinsi jeneza la daktari bingwa wa kutahiri linavyopaswa kuundwa. Kwa kuzingatia usiri na unyeti wa kiungo hicho kadiri ya maadili ya Watanzania, kusawiriwa kwake katika umbo la jeneza huweza kuleta mnato wa aina ya pekee katika akili ya mpokeaji; hivyo kuweza kusababisha ufutuhi. Tukio "**n**", kwa upande wake, usanaa wake umo katika namna neno "vua" lilivyotumika hadi kuweza kusababisha msigano katika akili ya mpokeaji. Utata wa kimaana katika neno hili ndio kiini cha kuwapo kwa msigano huo.

### 3.3 Ufutuhi kama Nyenzo ya Kupaza Ujumi wa Watanzania

Ufutuhi pia huweza kuwa nyenzo ya kutambulisha ujumi wa jamii husika. Dhana ya ujumi inatumiwa katika makala haya kumaanisha hali ya ufahari au thamani kuhusu uzuri au umaridadi utokanao na usanifu (kwa muktadha wa makala haya, ni ule usanifu uliomo katika matendo, uneni au hali za kifutuhi). Kwa kawaida, fikra za uzuri au umaridadi huenda pamoja na kinyume chake, yaani, ubaya. Ujumi unaoweza kubebwa katika ufutuhi ni ule unaojielekeza katika maadili na itikeli kulingana na mila na desturi za jamii; pamoja na ule unaojielekeza katika umbuji utokanao na matumizi ya kipekee ya lugha. Hisia hizo za kiujumi, kwa mujibu wa Bukenya na wenzake (2005) na Kiganza (2011), huweza kubainika katika matukio ya kifutuhi kwa kumakinikia vipengele vya wahusika, matendo, mandhari, miktadha, muundo wa kazi, maumbo ya kazi, lugha iliyotumika, pamoja na mwelekeo wa maudhui kutoka katika matukio hayo.

Watanzania wanao ujumi wao unaoongozwa na misingi mahususi pamoja na ile jumuifu. Ujumi huo ni miongoni mwa mihimili inayoshikilia na kuongoza aina na miegamo ya maarifa, fasihi, na sanaa zao nyinginezo. Aina na miegamo hiyo ya kiujumi, kwa hakika, huwa tofauti na ile inayoaminiwa au

kutumiwa na jamii nyinginezo. Mathalani, ni ujumi wa watu wa Afrika Mashariki, kama asemavyo Gorman katika Zirimu na Gurr (1973: 196), ndio ambao unawaongoza watunzi wajiulize kuhusu aina ya maudhui wanayopaswa kuyaelekeza kwa hadhira zao ambazo zimegawika katika matabaka mbalimbali. Miongoni mwa matabaka hayo ni lile linaloundwa na kundi dogo la wabobevu na wasomi, na lile kubwa linalowajumuisha wanafunzi wa ngazi mbalimbali na watu wazima wasio wabobevu wala wasomi. Pamoja na miongozo mingine, ujumi pia huwa na nguvu katika kutathmini na kuamua ni kundi gani linahitaji kazi zenye ufafanuzi wa kinadharia na kiitikadi; lipi linahitaji kazi zenye maelekezo; na lipi linahitaji kazi zenye viburudisho au mseto wa maelekezo na viburudisho. Ujumi huo hupazwa kwa kutumia mbinu na nyenzo mbalimbali. Miongoni mwazo ni hii ya ufutuhi. Kupitia maneno na matendo yenye vionjo vya kifutuhi ambayo wanajamii huyatumia katika mawasiliano yao, mtu huweza kubaini falsafa pamoja na ujumi wa jamii husika. Hii ni kwa sababu, kupitia hivyo vionjo vya kifutuhi, ni rahisi kubaini namna jamii husika inavyothamini vipengele kama vile maumbile, rangi na thamani ya matendo vilivyomo katika jamii yao.

Mathalani, mifano iliyodondolewa hapo juu inatuonesha jinsi jamii ya Watanzania inavyolithamini au kulipa kipaumbele suala la ngono mpaka kufikia kiasi cha kulisana kwa namna tofautitofauti. Zaidi ya asilimia 50 ya matukio yaliyodondolewa yameelekezwa katika suala la mapenzi na/au ngono (ama kwa kutaja sehemu za siri, matendo yatendwayo sehemu hizo au mazao yatokanayo na sehemu hizo). Utajaji huo waweza kuwa umefanywa kwa wazi au kwa kutumia jazanda. Mfano mzuri ni matukio “**a**”, “**b**”, “**d**”, “**e**” na “**g**”. Sura ya ndani ya tukio “**b**”, kwa mfano, inajielekeza katika utaalamu au ujuzi wa kufanya mapenzi “vizuri.” Dhana ya “kufanya mapenzi vizuri” ndiyo tunayoinasibisha na ujumi, hususani wa jamii za Watanzania.

### 3.4 Ufutuhi kama Kilainishi cha Maisha

Umaarufu na mahitaji ya ufutuhi yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku katika jamii ya Watanzania. Miongoni mwa sababu za mabadiliko haya ni kubadilika kwa mitindo ya kimaisha. Yumkini, hali ya maisha ya sasa inashinikizwa na misongo ya mawazo inayowakabili wanajamii kutokana na matatizo ya kimaisha (kiuchumi, kijamii, na ya kisaikolojia). Binadamu ni kiumbe mwenye silika ya ubunifu wa kukabiliana na mabadiliko yanayomzonga. Miongoni mwa nyenzo azitumiazo kukabiliana na matatizo hayo ni hii ya ufutuhi. Hii ndiyo sababu hasa inayofanya siku hizi kuwe na idadi kubwa ya programu za kifutuhi (Ponera, 2010). Programu hizi zinajumuisha zile zinazofanywa na mtu mmoja mmoja au za vikundi; za mitaani au za kwenye vyombo vya habari; zilizo maarufu na zisizo maarufu; na, zilizo ndani na nje ya miktadha ya kifasihi. Matokeo ya mwondoko huu mpya ni hali hii ya kuenea kwa matumizi ya

ufutuhi katika takribani nyanja zote za maisha. Mathalani, ni hali hii ndiyo inayoyasukuma mashirika ya televisheni yawe yanashindana kuandaa vipindi vya kifutuhi. Matokeo yake, tumefikia katika kipindi ambacho hata programu-dhati kama vile taarifa za habari "hulazimishwa" kuwa na ufutuhi, kiasi cha hata wakati mwingine kuichusha hadhira. Zaidi, ni mwondoko huu mpya ndio unaosababisha ufutuhi kuwa kionjo mashuhuri katika sehemu kubwa ya kazi za fasihi andishi na filamu za Kitanzania. Kwa mfano, ni jambo la kawaida siku hizi katika filamu za Kiswahili kuwaona mabawabu wakiwa wamevishwa uhusika wa kifutuhi hata wakati mwingine pasipo na ulazima wa kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa Billig (2005), Wamitila (2010) na Walibora (2013), mabadiliko ya mitindo ya kimaisha yanatokana na kani za kiwakati. Kipindi hiki cha baada-usasa (kama akiitavyo Wamitila (k.h.j) kimetawaliwa na matumizi ya kejeli (kijenzi kimojawapo cha ufutuhi). Kwa upande wake, Billig (k.h.j) anasema kuwa mwondoko huu mpya wa jamii kuipa umbele dhana ya ufutuhi unatokana na ukweli kuwa tumo katika jamii ambayo inaendeshwa na furaha na ucheshi katika takribani kila eneo la maisha ya mwanadamu. Walibora anaongezea kwa kusema:

> Fasihi haiwezi kuwa vilevile siku zote. Ni lazima iwe na mambo au namna mpya za kuweza kuifafanua. Kwa hivyo, sura hii ya fasihi ya sasa imechukuana vema na mwondoko wa maisha ya sasa. Hii ni kwa sababu kamwe Fasihi huwa haipitwi na wakati[1].

Hivyo basi, kutokana na hali hii ya kushamiri kwa matumizi ya ufutuhi katika jamii, ndiyo maana inatusukuma kuuona ufutuhi kama kiambata kilicho karibu sana na hali ya maisha ya sasa.

## 4.0 Hitimisho

Makala yamefafanua jinsi ufutuhi unavyojitokeza kwa jamii ya Watanzania; vilevile, imefafanua dhima zake. Matukio ya kifutuhi yaliyodondolewa yameonekana kuwa katika sura za ufyosi, kejeli, dhihaka na vijembe. Kuhusu dhima, makala haya yanafafanua dhima kubwa nne za ufutuhi ambazo ni: kuwa kiungo cha kijamii, kutekeleza sanaa au fasihi ya jamii husika, kielelezo cha ujumi, na kilainishi cha maisha ya sasa. Zaidi, makala yameonesha kuwa, ufutuhi hutegemea sana misingi ya kipokezi inayojiegemeza katika kiasi cha Hifadhi ya Maarifa aliyonayo mpokezi. Tofauti ya kiasi cha Hifadhi ya Maarifa

---

[1] Mahojiano baina ya mwandishi na Prof. Ken Walibora; yalifanyika Agosti 26, 2013 jijini Nairobi. Prof. Walibora ni mwananadharia na mtunzi wa kazi za kifasihi.

kati ya mpokeaji mmoja wa tukio la kifutuhi na mwingine ndiyo kiini cha kuwapo kwa tofauti ya kupatwa na ufutuhi kati yao.

**Marejeleo**

Attardo, S. (2001). *Humorous Texts: A Semantic and Pragmatic Analysis*. Berlin and New York: Mouton de Gruyter.

Bakhtin, M.M. (1984). *Problems of Dostoevsky's Poetics*. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Billig, M. (2005). *Laughter and Ridicule: Towards a Social Critique of Humour*. London: Sage Publications.

Bukenya, A.S., M. Wa-Gachanja & . Nandwa. (2005). *Oral Literature: A Senior Course*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Geybels, H. & W. Van Herck (Wah.) (2011). *Humour and Religion: Challenges and Ambiguities*. London: Continuum International Publishers Group.

Haiman, J. (1998). *Talk is Cheap: Sarcasm, Alienation, and the Evolution of Language*. New York Oxford University Press.

Janik, V.K. (1998). *Fools and Jesters in Literature, Art, and History*. Westport: Greenwood Publishers Group.

Kennedy, X.J na D. Gioia (2007). *Literature: An Introduction to Fiction, Poetry, Drama, and Writing* (Tenth Edt.). New York: Pearson-Longman.

Kiganza, P.M. (2011). "Ujumi katika Ushairi wa Mnyampala." Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Limbe, Z.D. (2012). "Mkabala wa Kibwege katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Tamthiliya ya *Amezidi* (1995) ya Said Ahmed Mohamed." Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lippitt, J. (1991). *Philosophical Perspectives on Humour and Laughter*. Durham thesis, Durham University.

Palmer, J. (1994). *Taking Humor Seriously*. London and New York: Routiledge.

Ponera, A.S. (2010). "Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji." Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ponera, A.S. (2014). "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban.

Robert na Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ross, A. (1998). *The Language of Humor*. New York: Routiledge.

Senkoro, F.E. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kauttu Limited.

Scheel, T. & C. Gockel (2017). *Humor at Work in Teams, Leadership, Negotiations, Learning and Health*. Gewerbestrasse: Springer.

Schuette, C. (2010). Gelatology, the Study of Laughter. Iliyosomwa tarehe 06/05/2016 katika http://www.bellaonline.com/articles/art38021.asp

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Wagner, P.C. (2007). *Lets Laugh! Discovering How Laughter Will Make You Healthy*. Shippensburg: Destiny Image Publishers Inc.

Walibora, mahojiano na mwandishi yalifanyika 26 Agosti 2013, jijini Nairobi.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Whipple, C. & S. Calvert (2008), "The Connection Between Laughter, Humour, and Good Health" katika Jarida la *Health Education Through Extension Leadership*. Kentucky: Kentucky University Press.

Zirimu, P. & Gurr, A. (1973). *Black Aesthetics: Papers from a Colloquium Held at the University of Nairobi, June 1971*. Nairobi: East African Literature Bureau.